TANGAZO LA SERIKALI Na. 56 la tarehe 26/1/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWAKATIKA ENEO LA NTANGANO YA MWAKA 2024

Jina

**1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Ntangano ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

**2.** Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

**3.** Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F2 yenye majira-nukta 564222MS, 9013803KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F3 yenye majira-nukta 565009MS, 9014070KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F4 yenye majira-nukta 565236MS, 9012908KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F5 yenye majira-nukta 564961MS, 9012690KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F6 yenye majira-nukta 564929MS, 9012349KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F7 yenye majira-nukta 564532MS, 9012321KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F8 yenye majira-nukta 564603MS, 9012884KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 1 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*